

Jina: Nambari Yako:

Sahihi Yako:

Tarehe:

Muungano KCSE Trial Exam

102/3

KISWAHILI

KARATASI ya 3

Fasihi

July 2017

Saa 2½

MAAGIZO:

Jibu maswali *manne*

Swali la *kwanza* ni lazima

Maswali *matatu* yaliyosalia yachaguliwe kutoka sehemu hizo zingine: *Fasihi simulizi, Riwaya,*

Tamthilia na *Ushairi*.

Usijibu maswali *mawili* kutoka sehemu moja.

Kila swali lina alama 20.

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.

Turn Over

SEHEMU YA A: Ushairi***Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata*****SIWE?**

1. Siwe ulosema jana, yakuwa u mashuhuri?
Ya kuwa wajuwa sana, aidha huna kiburi?
Nchini wajulikana, mwanasiasa mahiri,
Bungeni tukuajiri?
2. Siwe ulotushawishi, kwa chumvi na kwa sukari,
Na matamu matamshi , ukaziteka suduri,
Ukanena penya moshi, moto ndiyo yakwe siri,
Nawe ndiye hiyo nari?
3. Siwe uloji' ta moto, uwakao biribiri,
Kamba 'tatia fukuto, Litakalo leta kheri',
Utatufunua mato, Maisha yawe mazuri,
Tukupe kura waziri?
4. Siwe ulosema hayo, na mengi ukabashiri,
Ukamba wafata nyayo, nyayo ziso utiriri,
Tusiwe na wayowayo, wa kufikirifikiri,
Tukuachie ujari?
5. Siwe tulokuinua, Mabegani kama mwari,
Tungawa twalemewa, waume tukajasiri,
Kamba tukikuchaguwa, mema kwetu yatajiri,
Leo mekuwa hodari?
6. Siwe ulotugeuka, kwamba leo u waziri,
Wajiona melimuka, tena ukawa ayari,
Walaghai ukicheka, ukuu umekughuri,
Leo mekuwa hodari?
7. Siwe ulojawa raha, za hino yetu sayari,
Ukawa ja vile shaha, hatukupati shauri,
Kutuona ni karaha, wakatiwo twahasiri,
Ushakiya msitari?
8. Siwe uliyetughura, ukafunga na safari,
Ukaelekea bara, Kwa wenzio matajiri,
Ukatuachia majura, na tama kukithiri,
Kanama Ushaghairi?
9. Siwe uliyetuasi, ukenda pasi kwaheri,
Mbona hutwambii nasi, tukajua yetu shari,
Leo una masidisi, husemi na aso gari,
Ndio mezidi jeuri?

10. Siwe'lotwaa mgwisho, ukawa wajifakhiri?
Chenye mwanzo kina mwisho, hilo wajuwa dhahiri,
Vyaja kutoka vitisho, kwani hayo sidahari,
Mambo mengimdawari?
11. Siwe utakayeiza, mwishowo ukidhiri,
Siku itayoteleza, kija kwetu ansari,
Kuja kutubembeleza, kwa nyunga nalo khamri,
Tauya nazo nadhiri.

Maswali

- a) Mtunzi wa shairi hili *ana dhamira gani?* (al.2)
- b) *Taja* na *ueleze* bahari tatu za shairi hili? (al.3)
- c) *Onyesha kwa kutoa mifano*, mbinu tatu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (al.3)
- d) *Taja na ufafanue tamathali* ya usemi iliyotawala katika shairi hili (al.2)
- e) Anayerejelewa alibadilika vipi? *Eleza*. (al.3)
- f) *Andika ubeti* wa tisa kwa lugha ya tutumbi. (al.4)
- g) i) Bainisha toni ya shairi hili. (al.2)
- ii) Nafsineni katika shairi hili inasema na nani? (al.1)

SEHEMU YA B: Riwaya - Kidagaa Kimemwozea: Ken Walibora

Jibu Swali La 2 Au La 3

2. Kwa kurejelea riwaya ya kidagaa kimemwozea, *fafanua athari/matokeo mbalimbali* ya ELIMU kwa jamii ya Sokomoko. (al 20)
3. Pale kitandani Amani alimwangukia Imani kwa tabasamu. Alifurahi kumwona Imani. Alitaka kusema hivyo. Akashindwa.
- a) *Fafanua* muktadha wa dondoo hili (al 4)
- b) *kwa nini* Amani *alishindwa* kutamka yaliyokuwa moyoni mwake (al 2)
- c) *Eleza kwa ufupi* kilichosababisha na kumwelekeza Amani kitandani (al 2)
- d) *Tetea kwa kurejelea* Riwaya hii dai kuwa Amani alikuwa mwenye utu (al 12)

SEHEMU YA C: Mstahiki Meya: Timothy Arege

4 “Wafanyikazi katika bohari ya mafuta wamegoma”.

- (a) *Eleza muktadha* wa dondoo hili. (al 4)
- (b) *Toa sababu nne* kwa nini wafanyakazi wanagoma kulingana na muktadha huu. (al 4)
- (c) Wafanyakazi walifanya kazi kwa masaibu mengi kule Cheneo. Fafanua. (al 12)
5. Tamthilia ya Mstahiki Meya inaangazia hali halisi inayokumba nchi nyingi. Huku ukitoa mifano kumi, *thibitisha ukweli* wa kauli hii. (al 20)

SEHEMU YA D: Hadithi Fupi - Damu Nyeusi:

6. Ndoa ni asasi katika jamii iliyozungwa na matatizo chungu nzima. *Thibitisha ukirejelea hadithi zozote nne* za Diwani ya Damu Nyeusi. (al.20)

SEHEMU YA E: Fasihi Simulizi

7. i) Misimu *ni nini?* (al.2)
 ii) *Eleza sifa tano* za misimu. (al.10)
 iii) *Fafanua majukumu yoyote manne* yanayotekelezwa na misimu. (al.8)
8. a) *Eleza maana* ya miviga. (al.2)
 b) *Eleza sifa tano* za miviga. (al.5)
 c) Miviga *ina udhaifu gani?* (al.3)
 d) *Fafanua umuhimu* wa ngomezi katika jamii. (al.10)
 e) *Eleza vizingiti viwili* vinavyokumba ngomezi. (al.4)